



HALMASHAURI YA WILAYA LIWALE

Wilaya ya Liwale ilitawaliwa na wajerumani walijenga boma lao mnamo mwaka 1905 baada ya kupata uhuru 1961, wilaya ya Liwale ilikuwa tarafa wa wilaya ya Nachingwea. Julai 7, 1975 wilaya ya Liwale ilianzishwa baada ya kumegwa kutoka wilaya ya Nachingwea kutokana na ukubwa wa wilaya.

Wilaya ya Liwale ilikuwa halmashauri rasmi mwaka 1984 hapo ilikuwa na madaraka kamili kama yaliyoiinishwa katika sheria ya uanzishaji wa mamlaka hiyo ya mwaka 1982.



Ndani ya miaka 61 ya uhuru Serikali ya jamhuri wa Muungano wa Tanzania imefanya mabadiliko mbalimbali katika maeneo tofauti kama afya, elimu, miundombinu, huduma za jamii, na nishati. Wilaya ya Liwale imefikwa kwenye maeneo yote.

ELIMU

Wilaya ya Liwale ina jumla ya shule za msingi 72

Na mpaka mwaka 2022 kuna miradi mbalimbali ya ujenzi wa matundu ya vyojo katika shule za msingi, ujenzi wa nyumba za walimu. Kwa mwaka 2022 katika matokeo ya darasa la saba imeshika nafasi ya 3 kimkoa na Mkoa wa Lindi kushika nafasi ya 8 Kitafa.

Shule za sekondari zipo 17, kwa mwaka 2022/2023 180,000,000 zimepokelewa kwaajili ya ujenzi wa madarasa 9 ya kidato cha kwanza. Ujenzi wa maabara 30,000,000. Ujenzi wa bweni 50,000,000. Ujenzi wa bwalo la chakula. Hivyo kupitia miradi hii, elimu inakuwa kwa kasi na wananchi wanahamasika kupeleka watoto wao mashuleni. Hii kupeleka kukuza kizazi chenye elimu katika wilaya ya Liwale.

KAZI INDELEE

AFYA

Halmashauri ya wilaya ya Liwale imefanikiwa kujenga hospitali ya wilaya 1 vituo vya afya 2 zahanati 34, kwa mwaka 2021/2022 hadi 2022/2023 wilaya ya liwale ina miradi mitatu ya vituo vya afya katika vijiji vitatu; Barikiwa, Mirui na Nngongwele pia kwa mwaka 2022/2023 halmashauri imepokea 750,000,000 za ujenzi wa wodi 4. Umaliziaji wa zahanati ya Ngorongopa na Nanjejeja 100,000,000. Serikali imesaidia sana kuwezesha vituo vya afya na zahati katika uotoaji huduma bora kwa wagonjwa na kupunguza idadi ya vifo vinavyotokana na uzazi.




MIAKA 61 YA UHURU

Miundombinu

Wilaya ya Liwale ina barabara za kiwango cha changarawe ambazo zinaunganisha kati ya kata moja hadi nyingine.

Barabara ya kila inayunganisha nangurukuru mpaka Liwale kiwango cha changarawe, barabara hii ipo kwenye hatua ya upembozi yakiitua ili kujenga kiwango cha lami. Barabara ya Masasi Liwale kiwango cha changarawe, kuna barabara kiwango cha lami ambazo zinazunguka majini.

Madaraja ambayo yanaunganisha wilaya na wilaya, vijiji na vijiji. Miundombinu ya barabara imesaidia kua na ukwaji wa biashara na mwingiliano wa watu kutoka sehemu mbalimbali hii kupeleka ukwaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao na kuongezeka idadi ya watu.



UFUGAJI

Ndani ya miaka 61 ya uhuru serikali imejenga rambo yenye gharama ya 426,000,000. kwa ajili ya kuvuna na kutunza maji ya mvua kwaajili ya mifugo.

Wilaya ya liwale imetenga maeneo rasmi ya wafugaji.

SENSA

Idadi ya watu kwa sensa iliofanyika mwaka 2012
Jumla ya watu 91380

Idadi ya watu sensa ya mwaka 2022,
Jumla ya watu 136,505
Wanawake 67526
Wanaume 68979

UMEME

Moja ya mafanikio kutoka kutumia umeme wa jenereta mpaka kutumia umeme wa gas, umeme wa gas ulianza kutumika rasmi kuanzia tarehe 18.03.2019 Vijiji vyenye umeme ni 39, 37 vimeingizwa kwenye mradi wa rea awamu ya 3 mzunguko wa pili.

